



**MAMLAKA YA MAENDELEO YA BIASHARA TANZANIA  
(TanTrade)**



**TAARIFA KWA UMMA**

**UFAFANUZI JUU YA NAFASI YA MAMLAKA YA MAENDELEO YA BIASHARA  
TANZANIA (TANTRADE) KATIKA KUSIMAMIA SHUGHULI ZA UKUZAJI  
BIASHARA NDANI NA NJE YA NCHI**

**Dar es Salaam – 15 Novemba, 2022**

Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) ilianzishwa kwa Sheria Na. 4 ya 2009 baada ya kuunganisha Sheria Na. 15 ya mwaka 1973 (Sura ya 103 ya Sheria za Tanzania) iliyoanzisha Halmashauri ya Biashara ya Ndani (BIT) na Sheria Na. 5 ya mwaka 1978 (Sura ya 155 ya Sheria za Tanzania) iliyoanzisha Halmashauri ya Biashara ya Nje (BET). Aidha mwaka 2012, Sheria ya TanTrade ilifanyiwa marekebisho kwa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 3 ya 2012. Sheria hii ilitungiwa Kanuni zake mwaka 2010 zilizotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na.338 la 2010 pamoja na Kanuni za Uandaaji na Ushiriki wa Maonesho ya Kibiashara za mwaka 2014 (International Trade Fair (Terms for Organizers and Participation), 2014).

Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), pamoja na mambo mengine, imepewa jukumu la kusimamia shughuli za ukuzaji biashara nchini ikiwa ni pamoja na Maonesho na Misafara ya kibiashara.

Kifungu cha 5(1) (b) cha Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), Na. 4 ya mwaka 2009 pamoja na marekebisho yake, kimeipa TanTrade mamlaka ya kuunganisha na kudhibiti Soko la Ndani (Integrate and Regulate Domestic Market). Uratibu wa shughuli za Ukuzaji Biashara ni sehemu ya utekelezaji wa matakwa hayo. Kadhalika, Vifungu vya 5(1) (p), 5 (2) (e), vya Sheria hiyo, Aya ya 3(1)(k) ya Kanuni za Sheria ya TanTrade za mwaka 2010 pamoja na Jedwali la I la Kanuni za Uandaaji na Ushiriki wa Maonesho ya Kibiashara za mwaka 2014, vinaipa TanTrade mamlaka ya kumruhusu/ kutoa kibali kwa mtu yeyote, Taasisi au Shirika lolote kuandaa Maonesho ya ndani (local) na ya Kimataifa (International). Aya ya Aya ya 3 (1) (l) ya Kanuni za Sheria ya TanTrade za mwaka 2010, inaipa TanTrade mamlaka ya kuratibu Misafara ya Wafanyabiashara wanaoingia nchini na kwenda nje ya nchi (coordinating incoming and outgoing trade missions)

Kumekuwa na taarifa za upotoshaji kupitia mitandao ya kijamii kwamba TanTrade inatekeleza majukumu yake kinyume cha Sheria na kwamba inawanyima waandaaji vibali vya kuandaa shughuli za ukuzaji Biashara, jambo ambalo sio la kweli.

TanTrade inapenda kuisisitiza kuwa inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni, Sheria na Taratibu zilizowekwa na kwamba itaendelea kutoa vibali kwa watu binafsi, Kampuni, Taasisi na Asasi ambazo zimekidhi vigezo vya kuratibu shughuli za ukuzaji wa biashara bila kumwonea mtu yeyote.

Kadhalika tunatoa angalizo kwa Umma kuwa, ili kuepuka usumbufu usio wa lazima kabla ya kushiriki shughuli yoyote ya ukuzaji Biashara iliyoandaliwa na Kampuni au Taasisi yoyote, ni vema kupata uthibitisho ikiwa muandaaji amepata idhini ya TanTrade ya kuandaa shughuli husika.

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana nasi kupitia namba 0733 002 014 au tembelea tovuti yetu [www.tantrade.go.tz](http://www.tantrade.go.tz) au fika katika Ofisi zetu zilizopo katika Uwanja wa Maonesho wa Mwl. Nyerere, Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam au Jengo la Kilimo V, Barabara ya VETA nyuma ya CBE, Dodoma na Zanzibar, Kijangwani, Jengo la Posta.

Imetolewa na:

**Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano  
kwa Umma**